

Mikondo Mipya katika Utunzi wa Mashairi: Mifano Kutoka 'Sokomoko' na 'Ushairi Wenu' Katika Gazeti la Taifa Leo.

Nyongesa Salyne¹; Sheila Wandera-Simwa²; Wendo Nabea³.

^{1,2,3} Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya

Main author email: snnabangi@yahoo.com

IKISIRI

Utafiti huu unachunguza mikondo mipya katika mashairi yanayochapishwa katika gazeti la Taifa Leo, kumbi ya *Ushairi Wenu* na *Sokomoko*, katika kipindi cha Januari 1, 2018 hadi Agosti 31, 2019. Utafiti uliongozwa na nadharia ya kimtindo ya Leech na Short (2007) ili kuafikia lengo letu. Mihimili mitatu ya nadharia hii ilitumiwa ili kufanikisha lengo la mtafiti, nayo ni: Fasihi ni muundo wa lugha na kwa hivyo lazima matumizi ya lugha yazingatiwe, uhakiki wa kifasihi haupaswi kupuuzwa matumizi ya vipengele vya isimu lugha ikiwemo. Data iliyotumiwa katika utafiti ilikusanywa maktabani na mitandaoni kupitia usomaji wa tasnifu, vitabu, majarida na magazeti. Uteuzi sampuli wa kimakusudi ulitumiwa kuteua mashairi yaliyosheheni upya katika mikondo. Uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulifanywa kupitia kwa maelezo. Matokeo ya utafiti yalionyesha kwamba, mashairi ya ushairi wenu na sokomoko yanasheheni mikondo mipya ya utunzi ikiwemo: Matumizi ya Sheng', usimulizi na kuwepo kwa mianzo ya kifomula. Mashairi yaliyotumika yalitolewa katika kumbi za *Sokomoko* na *Ushairi Wenu* ambazo ni kumbi zinazochapisha mashairi ya watunzi mbalimbali katika gazeti la *Taifa Leo*. Matokeo ya utafiti yalionesha namna mikondo mipya ya utunzi inaendelea kuibuliwa na watunzi wa mashairi kila uchao. Mashairi yaliyotumika hapa hata hivyo, ni yale ya kiarudhi pekee kwani ndiyo yachapishwayo katika gazeti la *Taifa Leo*. Makala haya yatakuwa ya manufaa kwa walimu wa Kiswahili, wanafunzi na watafiti wengine wanaotafitia suala la upya katika utunzi wa mashairi.

Maneno Muhimu: Ushairi, mikondo, upya, ushairi wa gazetini

How to cite this article in APA (6th Edition)

Nyongesa, S.; Wandera-Simwa, S., & Nabea, W. (2020). Mikondo Mipya katika Utunzi wa Mashairi: Mifano Kutoka 'Sokomoko' na 'Ushairi Wenu' Katika Gazeti la Taifa Leo. *Editon Cons. J. Kiswahili*, 2(1), 188-198.

UTANGULIZI

Ushairi wa Kiswahili umepitia hatua nyingi za mabadiliko kiutunzi katika vipindi tofauti tofauti hadi ufikie hapa ulipo. Makala haya yamejikita katika kuangazia upya wa mikondo katika mashairi ya *Ushairi Wenu* na *Sokomoko* ambayo huchapishwa katika gazeti la *Taifa Leo*. Ushairi wa Kiswahili tangu awali umekuwa ukibadilika kifani na kimaudhui kutegemea na namna ambayo mtunzi atahisi ni njia bora ya kutumia mtindo fulani wa kuwasilisha maudhui yake. Onyanja (2015), anafafanua kuwa mikondo na mitindo mipya katika ushairi sasa ni sehemu ya historia ndefu ya ushairi wa Kiswahili ambapo watunzi wamekuwa wakiibuka na mikondo mipya ya utunzi. Mawazo ya mtaalamu huyu yanatiliwa mkazo naya Nyanchama (2004) anayesema kuwa mtunzi ana uhuru wa kuisuka kazi kazi ya shairi apendavyo. Jambo hili linadhihirika kupitia kwa watunzi hawa wa ushairi wa magazetini, kwani wametumia mikondo mbalimbali ambayo zamani haikuwa imezoeleka au kutumika na watunzi wengi wa mashairi. Mikondo mipya inabainika katika kazi za *Ushairi Wenu* na *Sokomoko* ambazo ni kazi za washairi wa sasa magazetini, Kazi zao zinadhihirisha mitindo inayokaribiana hata ingawa maudhui yanaweza kutofautiana au kufanana. Katika kuwasilisha maudhui yao, watunzi hawa wamechagua mikondo mipya katika uwasilishaji inayojitokeza kama njia mpya ya na hivyo kuthibitisha kuwepo kwa upya wa mikondo katika mashairi haya. Makala hii kwa hivyo inatambua na kufafanua upya wa kimikondo unaojitokeza katika mashairi ya *Ushairi Wenu* na *Sokomoko* yanayochapishwa katika gazeti la *Taifa Leo*.

MAPITIO YA MAANDISHI

Dhana ya Mikondo Mipya katika Utunzi wa Mashairi

Kabla ya kujadili na kuonyesha namna ambavyo mikondo mpya zinaendeleza historia ya ushairi wa Kiswahili ni vizuri tufafanue istilahi mikondo kama inavyotumika katika makala hii. Mikondo ni mwelekeo unaotawala kazi

ya fasihi katika kipindi fulani cha wakati. Upya katika utunzi wa mashairi ni uibukaji wa mitindo mbalimbali ambayo haikuzoeleka awali na watunzi tofautitofauti. Mitindo hii mipya tunayoiita mikondo mipya katika utunzi ni pamoja na mkondo wa matumizi ya sheng', mkondo wa usimulizi na kuwepo kwa mianzo ya kifomula.

Mikondo Mipya ya Utunzi wa Mashairi

Mikondo mipya mitatu ya utunzi ambayo ni mkondo wa sheng', mkondo wa usimulizi na mkondo wa fomula. Mikondo hii aidha inatokana na ubunifu wa watunzi unaochangiwa na mabadiliko yanayotokea na kuibuka mara kwa mara katika fasihi.

Misingi ya Kinadharia

Makala haya yaliozwa na nadharia ya kimtindo ya kirasimi iliyoasisiwa na wataalam kadhaa wakiwemo Barry, (2002), Paul Simpson (2004), na Leech na Short (2007). Nadharia hii inaelekeza kuwa mtunzi huwa na mawazo yaliyombwa akilini mwake na hivyo huwa na jukumu la kuteua njia bora ya kuwasilisha mawazo hayo. Uteuzi wa njia ya uwasilishaji hapa ndiyo inayozua mikondo. Wataalam hawa wanazidi kufafanua mihimili mbalimbali ya nadharia ya mtindo kama vile: Mtunzi wa kazi ya fasihi humezwa na mkondo wa fikra kuhusu mambo yanayomzunguka. Mhimili huu ulitufaa katika kuangazia namna mikondo mipya ya utunzi zinazoibuliwa na washairi mbalimbali wa *Sokomoko* na *Ushairi Wenu* wanavyosuka maudhui yanayochotwa kutokana na mazingira yao. Mhimili mwingine tulioutumia ni ule unaodai kuwa fasihi ni muundo wa lugha na sharti matumizi ya lugha yaangaziwe. Katika kazi hii inagundulika kuwa kanoni tulizojadili ni sehemu ya mtindo inayounda fani ambayo kwayo maudhui mbalimbali yameibuliwa. Aidha Simpson (2004), anafafanua mambo ya kimsingi yanayoelekeza uhakiki wa kisasa. Mambo haya ni lugha ya kitamathali na mtindo, uchimuji na mtindo, usimulizi na mtindo, ukiushi wa

kisarufi, ukiushi wa kilahaja, ukiushi wa kimsamiati na kadhalika. Katika kazi hii tulipata kuwa baadhi ya mikondo imedhihirisha kuwepo mageuzi katika msamiati, mtindo na hata lugha. Kwa hivyo uhakiki wa kisasa wa nadharia ya kimtindo ulitufaa katika kutambua mabadiliko haya na kutathmini upya katika mashairi haya.

Mikondo Mipya ya Utunzi katika Mashairi ya Ushairi Wenu na Sokomoko

Nadharia ya umitindo inaelekeza kuwa mwanasanaa anayetunga kazi ya kirasimi humezwa na mkondo wa fikira uliomzunguka. Mikondo hii huwepo na kuendelezwa na wasanii mbalimbali au kuibuliwa na kuendelezwa na watunzi tofautitofauti. Kwa hivyo, suala la kuwepo kwa mikondo isiyozoeleka na inayoibuka katika fasihi ni suala ambalo hutawala fasihi katika vipindi mbalimbali. Kutokana na hili, utafiti huu uligundua kuwepo kwa mikondo mipya inayoibusha upya katika sanaa ya ushairi wa Kiswahili. Mikondo hii ni pamoja na mkondo wa Sheng', mkondo wa usimulizi, mkondo wa mianzo ya sala na mkondo wa kifomula.

Mkondo wa Sheng'

Kwa mujibu wa Wamitila (2003), mkondo ni istilahi ambayo inajikita katika ushairi wa jadi kwa maana ya aina tofauti za shairi la bahari moja. Hata hivyo, mabadiliko ambayo ushairi wa Kiswahili umepitia umesababisha kuibuka kwa mikondo mipya ya utunzi wa mashairi. Mabadiliko haya yamefikia kiwango cha kutoka nje ya fasili hii kwani mkondo sasa ni suala lililopanuka na kuzidi fasili ya kuihusisha na bahari pekee. Kwa sababu hii, utafiti huu umefasili mkondo kama mwelekeo unaotawala kazi ya fasihi katika kipindi fulani cha wakati. Kwa miaka ya hivi karibuni kumekuwepo na ongezeko la matumizi ya sheng' miongoni mwa vijana. Suala hili limewafanya watunzi mbalimbali wa mashairi haswa vijana kuwa na haja ya kutunga mashairi kwa kuchopeka maneno ya sheng' ili kuifikia hadhira pana katika jamii haswa

ikizingatiwa kuwa ushairi sasa ni fasihi pendwa. Huu ni ubunifu unaoshuhudiwa kutoka kwa watunzi hawa na pia suala la mabadiliko yanayosababishwa na mazingira wanamopatikana watunzi mbalimbali. Nyanchama (2004) anasema kuwa watunzi wa kisasa wametumia ubunifu wao kuzuka na mikondo mipya ya utunzi wa mashairi. Mawazo haya yalikuwa ndiyo msingi wa utafiti huu. Utafiti huu unakubaliana na maoni ya mtaalamu huyu kwani ulifanikiwa katika kuonyesha namna washairi wameibuka na mikondo tofauti tofauti katika kubuni ujumbe wao katika *Ushairi Wenu na Sokomoko*.

MATOKEO

Sheng' katika Ukiushi wa Kisemantiki.

Ukiushi wa kisemantiki unachunguza maana ya maneno yalivyotumika katika ushairi na kwa kawaida washairi walitumia Kiswahili sanifu katika ukiushi wa maneno. Hata hivyo, katika muktadha huu, utafiti ulichunguza namna ambavyo baadhi ya maneno ya Sheng' yamepewa maana isiyoyawaida katika *Ushairi Wenu na Sokomoko*. Katika shairi *Mgema Sifurahishe* lililochapishwa Sokomoko tarehe 27, Januari 2019, Kulikuwa na neno *mapuya* ambalo lina maana ya pombe aina ya busaa. Neno hilo limetoa maana ya pombe aina ya busaa bila kuitaja busaa yenyewe hasa. Hili ni neno la Sheng' linalofahamika na vijana mitaani. Mtunzi ametumia ubunifu wake ili kutoa maana kwa hadhira lengwa. Busaa ni mojawapo ya vileo vilivyoorodheshwa kuwa haramu na shirika la kupambana na dawa za kulevya na vileo humu nchini (NACADA 2013).

Ubeti wa 2

*Kanunu ni mithilisha, mja soni nitwikiwa,
Mararururu nivisha, dhariri umeshakuwa,
Hela ulizokopesha, mapuya kuyabugia,
Baba wajibika sana, mgema sifurahishe.*

Muguka ni neno lingine ambalo limejitokeza kuwa la Sheng' katika mashairi yanayochapishwa Ushairi Wenu na

Sokomoko. Limetumiwa mara si moja na watunzi tofauti tofauti. Katika ukumbi wa *Ushairi Wenu* 19, Januari 19, 2019 shairi lenye mada *Ipigeni Marufuku* lilisheheni neno hili. *Muguka* ni aina ya majani ya miraa yanayotafunwa. Shirika la kupambana na matumizi ya dawa za kulevya nchini limeorodhesha miraa kama mojawapo ya dawa za kulevya. *Muguka* kwa hivyo ni dawa ya kulevya nchini Kenya. Jina hili la *muguka* linatumiwa haswa na vijana na watu wazima kote nchini. *Muguka* ni jina lililozoeleka baada ya kukosekana kwa tafsiri yake kwani asili kamili ya neno hili ni sehemu za Mbeere kaskazini na kusini ambapo zao hili hukuzwa kwa wingi. Katika mfano huu, neno *Muguka* limerudiwarudiwa. Kurudiwarudiwa kwa neno hili kunatoa msisitizo unaoonyesha kuwa miraa imekuwa na athari hasi katika jamii.

Ubeti wa 1

*Sio maneno ya siasa, ni ya kweli yashikeni,
Muguka hapa Mombasa, marufuku ipigeni,
Imeharibu kabisa, hata watoto shuleni,
Muguka hapa Mombasa, marufuku ipigeni.*

Mtunzi anapendekeza kupigwa marufuku kwa miraa jijini Mombasa. Neno hili limetolewa katika lugha ya kiasili (Kiembu) na kutumiwa kama Sheng' bila kubadilisha umbo lake wala maana ya matumizi. Mfano huu unadhihirisha kuwa maneno ya Sheng' sasa si lazima yatumie muundo wa awali wa kuchanganya silabi za Kiingereza na Kiswahili bali pia inaweza kukopa maneno kutoka lugha za kiasili na kuyapa maana hiyohiyo katika Sheng'. Aidha neno hili halitumiki katika lugha hiyo ya kiembu kama sheng'. Neno hili linapobadilisha mazingira kutoka lugha ya Kiembu hadi Kiswahili ndipo linakuwa sheng'. Maana yake pia haibadiliki ila inasalia kuwa ni ile inayorejelea miraa. Kutumika kwa maneno kama haya katika mashairi kunatokana na sababu mbili. moja ni kuwa baadhi ya watunzi wameathirika mno na mazingira wanamoishi hivi kwamba inakuwa ni vigumu kujitenga na

namna ambavyo lugha inatumiwa. Hapa ina maaana kuwa baadhi ya watunzi wa mashairi wameathirika na sheng kwani inatumiwa mno kule wanakoishi. Pili ni kuwa watunzi hawa wana ufinyu wa msamiati wa Kiswahili suala linalowafanya kutumia maneno ya sheng katika kazi zao mbalimbali. Inawezekana pia kuwa ufinyu huu unatokana na suala la kuwepo msamiati finyu wa baadhi ya maneno haya yanayotoka katika lugha zingine na kukosa tafsiri.

Sheng' na Nahau.

Wamitila (2003) anafafanua nahau kama misemo inayofafanua maana iliyofichika. Kulingana naye, nahau ni misemo inayopatikana katika lugha fulani. Mara nyingi nahau huundwa na kitenzi jina. Vilevile, Msokile (1993) anasema kuwa nahau ni msemu uliojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida, aidha aghalabu huwa umesitiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno ya nahau yenyewe. Suala la matumizi ya nahau limekuwepo katika mashairi ya Kiswahili kwa kutumia lugha sanifu, ila sasa hivi watunzi wameanza kutumia sheng' kuunda misemo na nahau ya sheng'. Mifano kadhaa katika *Ushairi Wenu* na *Sokomoko* inadhihirisha hili. Shairi la *Hayakuwako zamani*, lililochapishwa *Sokomoko* tarehe 27, Mei 2019 linathibitisha kauli kwani lina kifungu cha Sheng' katika utao wa mshororo wa tatu katika ubeti wa tano '*pombe kibao mtungi*' mbali na neno lenyewe katika utao wa mshororo wa kwanza wa ubeti uo huo. Maneno haya ni ya kawaida lakini yamebeba maana ya ndani iliyofichika.

Ubeti wa 5

*Kwetu hakuna amani, sababu ya mairungi,
Wengi huwa visirani, wakiongeza na bangi,
Tena aweke tumboni, 'pombe kibao mtungi',
Hayakuwako zamani, tunayo ya siku hizi.*

Utao '*Pombe kibao mtungi*' una maana ya pombe kiwango kingi ambacho mtumiaji amekunywa. Ni dhahiri kusema

kuwa Sheng' katika shairi hili imetumiwa pakubwa kiasi cha kubuni nahau kwani inatoa maana tofauti na maneno yaliyotumiwa. Inadhihirika kuwa Sheng' imeibusha nahau na misemo ambayo vilevile inatumiwa na watunzi katika mashairi yao. Kutumiwa kwa misemo ya Sheng' katika mashairi ya Kiswahili ni suala geni na ambalo halijazoeleka. Ni katika kipindi hiki cha sasa ambapo suala kama hili linaibuka kama tunavyoona katika mfano huu.

Sheng' na Ukopaji

Ukopaji ni hali inayojumuisha uhamishaji wa kipashio fulani kutoka lugha moja hadi katika lugha nyingine. Kwa hivyo, ukopaji huhusisha lugha mbili: kuna lugha chagizi na lugha pokezi, (Jefwa 2010). *Muguka* ni neno la Sheng'. Neno hili limetumika mara si moja na watunzi tofauti tofauti. Kwa mfano katika ukumbi wa *Ushairi Wenu* 19, Januari 19, 2019 shairi lenye mada *Ipigeni Marufuku* lilisheheni neno hili. *Muguka* ni aina ya majani ya miraa yanayotafunwa. Vijana ndio wameipa miraa jina hili baada ya kukosa tafsiri yake kwani asili yake kamili ni kutoka lugha ya Kiambu. Aidha neno linapotumika katika lugha ya kiambu si sheng kwani ni msamiati halisi wa lugha hiyo. Neno hili linapobadilisha mazingira na kuingia katika Kiswahili basi linatumika kama sheng' haswa katika miji ya Nairobi na Mombasa.

Ubeti wa 1

*Sio maneno ya siasa, ni ya kweli yashikeni,
Muguka hapa Mombasa, marufuku ipigeni,
Imeharibu kabisa, hata watoto shuleni,
Muguka hapa Mombasa, marufuku ipigeni.*

Neno hili limetolewa katika lugha ya kiasili (Kiambu) na kutumiwa kama Sheng' bila kubadilisha umbo lake wala maana ya matumizi. Hapa kwa hivyo, Kimeru ni lugha chagizi na msimbo wa sheng ni lugha pokezi. Mfano huu unadhihirisha kuwa maneno ya Sheng' sasa si lazima yatumie muundo wa awali wa kuchanganya silabi za

Kiingereza na Kiswahili bali pia yanaweza kukopa maneno kutoka lugha za kiasili na kuyapa maana hiyo katika Sheng'. Maneno haya yanapewa maana bila kubadilisha maumbo yake kutoka lugha moja yaani ya kiasili ambapo neno limekopwa hadi lugha nyingine. Kwa mfano, katika neno hili linatumika kwa maana ya miraa kama inavyofahamika katika lugha ya Kiambu. Ina maana kuwa neno limebadilisha mazingira na kutumiwa kama sheng' katika Kiswahili.

Sheng' na Mipinduo ya Kisintaksia

Mipinduo ya kisintaksia si jambo geni katika ushairi wa Kiswahili. Hata hivyo, kufungamanishwa kwa mipinduo hii na sheng ndiko kunakoifanya kuonyesha upya ndani mwake. Mipinduo ya kisintaksia imekuwa ikitokea kupitia uborongaji wa sarufi katika ushairi wa magazetini. Katika mashairi ya hapo awali tunaona jambo hili likisheheni pia. Hata hivyo, mashairi ya sasa yanatumia sheng kufanikisha matumizi ya mipinduo ya kisintaksia. Wamitila (2008) anadai kuwa kuboronga kwa sarufi kunajumuisha sentensi, vishazi na hata virai kwa namna inayokwepa muundo wa kawaida utumikao katika lugha. Ukiushi wa mipinduo ya kisintaksia hutumiwa na watunzi ili kulinganisha vina na pia kudumisha sajili ya ushairi. Watunzi wa *Ushairi Wenu* na *Sokomoko* wametumia baadhi ya mikondo ya ukiushi wa kisintaksia wenye upya wa kutumia maneno ya lugha ya Sheng'. Mifano inajitokeza katika mashairi ya *Sokomoko* Julai 8, 2018, ambapo mashairi mawili tofauti yalikuwa na maneno ya Sheng'. Shairi la kwanza lilikuwa *Maisha haya* na neno aliloliumia mtunzi katika utungo wake lilikuwa "ushagoni" lililorefushwa kutokana na neno 'ushago' lenye maana ya *shambani* au *kijijini*. Mazida ni mbinu ya kurefusha baadhi ya maneno kwa lengo la kupata urari wa mizani. Vilevile kuwezesha kudhibiti uwiano wa mdundo katika ushairi. (Mazrui, na Syambo (1992).

Ubeti wa pili

*Maisha yasiliani, mjini hadi shinani,
Siulize ya mjini, Zeki kwetu ushagoni,
Nimewaza kitanzini, hata sumu mawazoni,
Zeki sichoke tuliza, maisha haya yaishie.*

Neno lilivyotumika katika shairi linaingiliana vizuri na maneno mengine. Mshairi analalamikia ugumu wa maisha kwote iwe mjini ama mashambani, anakotoka anakokuita “ushagoni”. Kutokana na idhini ya mshairi, neno la kimsingi ‘ushago’ limerefushwa ili tupate usawa wa vina kwa kuongezwa silabi ‘ni’. Aidha neno hili ni Sheng’ lenye maana ya kijijini.

Kutokana na mifano hii ni dhahiri kuwa neno la Sheng’ ushagoni pamoja na mengine yaliyotumika katika mashairi mengine yanakidhi hitaji la kusawazishwa kwa mizani na vina. Wala hapana neno lilozidisha ama kupunguza idadi ya mizani na kuufanya mshororo wa ubeti wowote kuwa dhaifu. Vina vilevile havijaborongwa kwa maneno ya Sheng’. Kutokana na kusawazishwa kwa vina na baadaye mizani kisha mawazo ya watunzi yakaungwa pamoja na kutiririka kutoka mshororo mmoja wa ubeti mmoja hadi mwingine mtafiti alipata kuwa washairi wanaotumia Sheng’ wameafikia suala la utoshelevu ambao wanajadi walilienzi mno. Kwa ujumla, Sheng’ imetumiwa na washairi wa sasa kukuza utoshelevu.

Mkondo wa Mianza

Mashairi ya *Ushairi Wenu na Sokomoko* yamedhihiri upya wa mianza ndani mwake. Upya unaojitokeza katika mkondo huu unadhihirika kwa njia mbili. Moja kuna mashairi yanayoanza kwa mianza ya sala na pili mashairi yanayoanza kwa fomula ya kutanguliza kama ilivyo katika hadithi na ngano. Ni vizuri kutambua kuwa mianza hii imekuwepo tangu awali. Hata hivyo, namna washairi wa sasa wanavyotumia mianza hii ni tofauti na hapo awali suala linaloifanya mianza hii kudhihirisha upya ndani

mwake. Mkondo huu kwa hivyo, umezuka na upya unaoonyesha upekee wa kazi za watunzi wa mashairi ya magazetini.

Mianza ya Sala

Katika ushairi wa jadi, Muyaka Bin Haji alihusishwa na utoaji wa ushairi wa Kiswahili msikitini na kuuleta sokoni. Mageuzi haya yaliwafanya watunzi kujitenga na maudhui ya kidini hasa matumizi ya dua katika mashairi yao. Washairi wa jadi walioishi kabla ya Muyaka walitanguliza kazi zao kwa sala na hata kumaliza kwa sala. Hata hivyo, ni vizuri kutambua kuwa jadi, tenzi zilizotungwa zilikuwa na mianza ya maombi katika beti kadhaa kabla ya ujumbe mkuu au dhamira ya mshairi kuafikiwa. Baadaye, kulifuata usimulizi na kisha viishio vilivyokuwa na sala nyingine. Hili lilikiukwa pakubwa baada ya mageuzi haya yaliyoletwa na Muyaka kwani washairi tena hawakutaka kuhusisha kazi zao na suala la dini. Hata hivyo, suala hili limebadilika karibuni kwani sasa suala la mianza ya sala limerejea na linatumika sana na washairi wa *Ushairi Wenu na Sokomoko*. Hata hivyo, kuna upya ambao unajitokeza katika mianza hii. Mosi, mashairi ya sasa yenye mianza ya sala hayafungwi kwa sala. Mashairi haswa utenzi wa awali ulikuwa na mianza ya sala na kukamilishwa kwa sala. Mashairi ya *Ushairi Wenu na Sokomoko* yanadhihirisha kuwepo kwa upya huu. Mashairi haya yenye mianza ya sala yanahitimishwa bila sala. Mfano, shairi mpenzi nipe *kibali* lililochapishwa *Sokomoko* Januari 21, 2018, mshairi huyu amechukua mkondo wa kuanza kazi yake kwa sala.

Ubeti wa 1

*Bismilahi naanza, kwa jina la mwenyezi,
Peupe natangaza, habibi sikuchezi,
Daima sitosaza, kuonesha langu penzi,
Mpenzi nipe kibali, niwe wako wa sudiri.*

Ubeti wa mwisho

Beti nne kaditama, kikomo hapa natia,

*Ewe wangu wa mtima, habibi nashadidia,
Tupigane makamama, nipate kufurahia,
Mpenzi nipe kibali, niwe wako wa sudiri*

Mshairi anaanza kwa maombi kwa kutaja kuwa anatambuliza utunzi wake kwa jina la Mwenyezi Mungu. Anasema kuwa ni kwa jina lake ndiposa anatoa utungo wake. Mshairi huyu hajahitimisha kwa sala kama walivyofanya washairi wa awali ambao walihitimisha kazi zao kwa sala. Ubeti wa mwisho wa shairi hili haumalizi ujumbe wa shairi kwa sala. Mfano huu unathibitisha kuwepo kwa upya huu wa kuanza kwa sala na kutohitimisha kwa sala katika shairi tofauti na ilivyokuwa awali. Pili, baadhi ya washairi wanaanza kwa sala katika mishororo kadhaa katika ubeti na kutumia mishororo mingine katika ubeti huo huo kuwasilisha ujumbe.

Mkondo huu unaonekana kuwa na nguvu kwani umetumiwa sana na washairi hawa wa Ushairi Wenu na Sokomoko. Mianza ya sala inazua mambo kadhaa. Moja, ni kuwa watunzi wanaitumia kama njia mojawapo ya kutoa shukrani kwa Mwenyezi Mungu kwa kuwakirimia kipaji cha utunzi. Pili, wanaitumia kumwomba Mungu awajalie katika utunzi wao. Wengine wanatambuliza kwa kumtaka Mungu radhi kwani watakayoyanena huenda yasimfurahishe na mwisho Mungu awape mwelekeo mwema wa kutunga mambo yenye mashiko na busara katika jamii. Kutaka kutunga kazi yenye mashiko katika jamii kunaonyesha namna watunzi hawa wanavyoenzi maadili katika jamii. Hili linaingiliana sambamba na mhimili wa nadharia ya uhalisia unaodai kuwa matukio katika fasihi huakisi hali halisi katika jamii. Washairi wa Ushairi Wenu na Sokomoko wamejizatiti kuafikia hili. Hivyo basi, kuasi mageuzi yaliyotokea enzi za Muyaka kunaonesha kuwa washairi wa sasa wamerejelea mtindo wa awali wa utunzi ambapo wanatambuliza kwa sala kazi zao licha ya kuzua upya wa namna fulani.

Mianza ya Kifomula

Mkondo huu ni ule unaotumia fomula ya kufungua kama tuonavyo katika hadithi au masimulizi. Kupitia mkondo huu tunaona mwingiliano wa tanzu ukijitokeza kwani katika ushairi wa magazetini suala la washairi kutumia fomula ya ufunguzi sawia na usimulizi lipo. Aidha, ni vizuri kutaja kuwa tuliangazia mkondo huu tofauti na mkondo wa usimulizi kwa kuwa suala la kuwepo mianza ya kifomula katika mashairi haya linachukua mkondo huu; kwamba shairi linaweza kuwa na usimulizi na likatumia fomula ya ufunguzi. Lakini mashairi mengi ya Ushairi Wenu na Sokomoko yanaweza kuwa na fomula ya kufungua na yakakosa usimulizi ndani yake. Hili ni suala ambalo halikushuhudiwa awali katika mashairi ya Kiswahili. Mashairi yafuatayo yanaithibitisha kauli hii.

Machi 10, 2018 shairi *Nawaletea salamu* lilichapishwa katika ukumbi wa Ushairi Wenu. Shairi hili lilikuwa na fomula ya kufungua. Ubeti wa kwanza ulianza kwa kuelezea kuwa mshairi alikuwa ameishika *kalamu*. Kauli hii inamfahamisha msomaji wa shairi kujua kuwa mshairi alikuwa anaiandaa hadhira yake kabla ya kuwasimulia shairi.

Ubeti wa 1

*Nimeishika kalamu, nashukuru ni mzima,
Nawaletea salamu, wazazi baba na mama,
Ili mpate fahamu, nilipo niko mzima,
Nawaletea salamu, wazazi baba na mama.*

Mwanzo huu ulitambuliza kwa kuwataja wahusika yaani nafsi nenewa ambao ni baba na mama yake mtunzi. Baada ya ubeti huu, beti zinazofuata zinafafanua kiini cha mshairi kutunga shairi hili bila usimulizi wowote. Huu ni ukiukaji wa mtindo wa awali wa utunzi uliohusisha fomula hii. Sasa ni wazi kuwa mshairi hachukui ubeti mzima kutambuliza lakini mishororo michache tu au hata mmoja pekee. Pia kuna kupunguzwa kwa usimulizi katika kazi hii

yenye fomula ya kutanguliza ndani mwake. Sasa mashairi yenye fomula ya kutanguliza yanafafanua maudhui moja kwa moja bila kusimulia vitushi vingi. Maudhui kwa hivyo, yanawasilishwa moja kwa moja. Mfano mwingine ni shairi *Ushuru watafunwa* lililochapishwa Julai 29, 2019 Sokomoko. Shairi hili lilikuwa na fomula ya kufungua yenye upya ndani mwake. Ubeti wa kwanza unaanza kwa kuitaka hadhira kumsikiliza anaposema *Pulika wenzangu...* Katika mshororo wa kwanza wa ubeti huo.

*Pulika wenzangu, mwananchi nimefika,
Naleta kilio changu, kilio cha uhakika,
Nalisuta hili wingu, ambalo limetuteka,
Ushuru wangu jamani, unaliwa na mwingine.*

Mbali na kutanguliza kwa fomula, mshairi anaeleza msingi wa kutunga shairi. Kwamba anataka kueleza kuhusu jinsi ushuru unavyotumiwa visivyo na wafisadi. Anaendelea katika beti zingine kuelezea namna ushuru wake unavyofujwa na watu mbalimbali serikalini. Katika shairi hili ni mshororo wa kwanza katika ubeti huo wa kwanza ndio unaotanguliza kwa fomula. Fomula hii inateka makini ya hadhira na kuifahamisha kuwa kuna usimulizi uaofuata na baada ya kifungu hicho kunafuata mawazo ya mtunzi. Misingi ya awali ya kuwa na ubeti mzima unaokuwa fomula kwa hivyo unakiukwa. Msingi mpya unajitokeza kuwa: mshororo mmoja au hata kipande cha mshororo mmoja kinaweza kusimamia fomula nzima ya kufungua. Pia, mashairi mengi ya sasa yenye kutumia mianzo ya kifomula hayalazimiki kufungwa kwa fomula. Mashairi yanaanza kwa fomula na kuisha bila kufungwa kwa fomula ya aina yoyote ile, hili linazua taharuki mno ya ikiwa je, ujumbe aliokusudia kuuwasilisha mtunzi umekamilika?

Mkondo wa Usimulizi

Muchiri (2016) akiwanukuu Walleck na Warren (1986) anasema kuwa katika utenzi, mtunzi husimulia kisa kama

msimulizi wa nafsi ya tatu. Wakati mwingine huwapa nafasi wahusika wake kuzungumza moja kwa moja. Wanaendelea kusema kuwa wahusika katika shairi husemezana. Hii hujitokeza haswa katika mashairi ya malumbano. Wanasema kuwa usimulizi wa matukio waweza kuwa wa nafsi ya kwanza na ya tatu. Hata hivyo, katika utafiti huu tunaona kuwa usimulizi wa nafsi ya pili ukijitokeza suala linalofanya mashairi ya magezetini kusheheni upya. Mifano ifuatayo inaonesha utokeaji wa usimulizi wa aina hii katika ushairi wa sasa gazetini. Mfano wa kwanza unatoka Sokomoko. Shairi hili linaitwa *Mwandani Bevalini*. Hili lilichapishwa Juni 24, 2019. Mshairi huyu ametumia usimulizi kuelezea tabia za mpenzi wake Bevalini.

Ubeti wa 1

*Ninaye wangu mwandani, wa kukuza urafiki,
Yu liposhe Bevalini, mimi naye marafiki,
Maneno yake moyoni, matamu mithili siki,
Nyota ya jaha usoni, Bevalini wapepea.*

Ubeti 2

*Kwa kweli umeumbika, Rabuka halaumiki,
Kisura u malaika, nakupea mia maki,
Kuwepo kwako baraka, liye juu kubariki,
Nyota ya jaha usoni, Bevalini wapepea.*

Ubeti wa 5

*Mja asikugeresha, rafiki ukampotea,
Wanaume wanapotosha, wosia ombi sikia,
Swahibu sitaki presha, kaburini kafikia,
Nyota ya jaha usoni, Bevalini wapepea.*

Mshairi ameanza kwa kusimulia kuwa anaye mwandani wake kwa jina Bevalini. Huyu mpenzi wake amemganda moyoni na hata anatoa mfano wa uzuri wake kuwa kama siki. Katika ubeti wa pili anasimulia umbile lake na sura. Anaeleza kuwa mpenzi wake ni mrembo mfano wa

malaika na kumpa asilimia mia moja juu ya mia moja kutokana na urembo wake. Katika shairi hili usimulizi wa nafsi ya pili unatokea katika ubeti wa pili mshororo wa kwanza katika *ukwapi kwa kweli umeumbika*, kuna utajaji wa nafsi ya pili unaotambulishwa na kiambishi -u-. Hili ni suala ambalo lilishuhudiwa kwa uchache mno kwa watunzi wa awali. Watunzi wa sasa wamejizatiti kulikuza. Mbinu hii inaufanya usimulizi kujumuisha uhusika nafsi kwa ukamilifu. Sasa mhusika wa nafsi ya pili anapata nafasi katika masimulizi na hivyo kukuza matukio na maudhui yaliyokusudiwa. Shairi *Uzee sasa watuchekea* lilichapishwa Machi 16, 2019 katika ukumbi wa Sokomoko. Kunao wahusika wawili katika shairi hili; baba na mtoto. Baba anamsimulia mwanawe mambo kadha kwa kumsimulia kule ambako ametoka, yani alivyopambana ili kumsomesha mwanawe, hivyo kudhihirisha upya kwa kutumia usimulizi wa nafsi ya pili.

Ubeti wa 1

*Mwanangu kaniskie, niendayo kukwambia,
Machache unakilie, uweze kuyatumia,
Wenzako wasikulie, na wewe wafurahia,
Kumbuka ulikotoka, watu uwasaidie.*

Ubeti wa 2

*Babako kukusomesha, mengi niliyapitia,
Katika yangu maisha, mema nilikuwazia,
Uje kutubadilisha, wazazi wako sikia,
Sasa umetusahau, kumbuka ulikotoka.*

Ubeti wa pili unataja jinsi mwanawe baba huyo amekengeuka na kuwasahau. Amesahau hata kaka na dada zake ambao wanamtegemea. Baba anasimulia kuwa katika kumsomesha mtoto mwenyewe alidhikika na lengo lake lilikuwa kumsomesha ili apate kuwakwama kama familia. Ndiposa anamkumbusha kutosahau lengo lao la kuweza kuwakomboa. Katika ubeti wa tatu anaeleza dhiki ambayo inawakabidhi kwa kuwa uzee

umewafakamia. Sasa hawawezi tena pamoja na mamake kwenda kulima. Hawawezi tena kudamka kama ilivyokuwa awali. Katika ubeti wa pili mshororo wa pili mgao wa kwanza kuna utajaji wa nafsi ya pili katika neno unakilie. Utajaji wa nafsi hii unaleta dhana ya uhusika katika shairi hili. Tofauti na awali, shairi kama hili linaonyesha kuwa nafsi ya pili inaweza kushughulikiwa katika kazi ya ushairi. Nafsi hii inawasilisha mawazo ya mtunzi bila kuvuruga mpangilio wa shairi au arudhi za utunzi wa mashairi. Maudhui vilevile yanajengeka tangu ubeti wa kwanza hadi wa mwisho. Hata katika vipera vingine vya fasihi ni wazi kuwa kukuza usimulizi wa nafsi ya pili umekuwa nadra sana tofauti na inavyotokea katika mashairi ya magazetini. Usimulizi wa nafsi ya pili haujavuruga mtindo wa kuwasilisha maudhui wala sheria za utunzi wa mashairi. Badala yake umeibua mbinu mpya ya uwasilishaji mawazo mbalimbali ya watunzi wa mashairi.

Hitimisho

Ni bayana kuwa mikondo mipya katika utunzi wa mashairi inatokana na ubunifu ambao waandishi wanaendelea kuzua wakati baada ya mwingine. Mabadiliko haya yanazuka sambamba na mabadiliko katika lugha, utamaduni na teknolojia. Muhimu kufahamika ni kuwa upya huu unajengwa kwa mikondo ya awali inayoelezwa na kusukwa kwa namna inayozua upya wa aina fulani. Mikondo hii ni pamoja na mkondo wa sheng', mkondo wa mianzo na mkondo wa usimulizi. Mkondo wa sheng' unatumia ukiushi wa kimsamiati, mipinduo ya kisintaksia, utohozu na ukopaji. Mkondo wa usimulizi unatumia usimulizi wa nafsi ya pili ambao awali ulikuwa nadra kuonekana katika kazi ya fasihi kwa ujumla. Mkondo wa mianzo una mianzo miwili: mwanzo ni mianzo ya sala na pili ni mianzo ya kifomula. Hii ni fomula ya kufungua. Kupitia mikondo hii, mashairi ya magazetini yamepata upya wa kimaumbo hata ingawa arudhi za utunzi hazijavurugwa.

Mapendekezo

Utafiti unapendekeza utafiti zaidi kufanywa haswa katika kulinganisha na kulinganua upya wa mikondo unaojitokeza katika mashairi yanayochapishwa magazetini au ushairi pendwa na upya wa mikondo katika ushairi dhati.

Pia utafiti unapendekeza utafiti katika mageuzi ya mara kwa mara katika utanzu wa ushairi wa Kiswahili kuendelea kufanywa.

MAREJELEO

- Abedi, K. A. (1954). *Sheria Za Kutunga Mashairi Na Diwani Ya Amri*. Nairobi: East African Literature Bureau.
- Harries, L. (1962). *Swahili Poetry*. Oxford. Clarendon Press.
- Jefwa, G. (2010). *Utangulizi wa Isimu*, Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Kezilahabi, E. (1983). *Historia fupi ya ushairi wa Kiswahili*, Dar es Salam: makala ya semina ya waandishi III.
- Knappert, J. (1972). *An antology of Swahili Love Poetry*. Berkeley. University of Carlifonia Press.
- Leech, G. N. & Short, M. H. (2007). *Style in Fiction: A linguistic Introduction to English Fictional Prose*. (Second edition). London.
- Mayoka, J. M. (1986). *Mgogoro wa Ushairi na Diwani ya Mayoka*. Dar es Salam: TPH
- Mazrui, A., na Syambo, B. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi* Nairobi: East Africa Education Publishers.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Msokile, M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Muchiri, A. W. (2016). *Fani katika utenzi wa Mwaka Hasina na Rashid Walii* (Tasnifu ya uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi, Kenya (hajichapishwa).
- NACADA (2013). *Trends and Patterns of Emerging Drugs in Kenya: A case study in Mombasa and Nairobi Counties 2013*.
- Nation Media Group (2018) *Taifa Leo Machi 3*, 2018. Nairobi.
- _____ (2018) *Taifa Leo Machi 10*, 2018. Nairobi.
- _____ (2018) *Taifa Leo Julai 22*, 2018. Nairobi
- _____ (2018) *Taifa Leo Mei 20*, 2018. Nairobi.
- _____ (2019) *Taifa Leo Mei 21*, 2019. Nairobi.
- _____ (2019) *Taifa Leo Januari 19*, 2019. Nairobi.
- _____ (2019) *Taifa Leo Mei 27*, 2019. Nairobi.
- Nyanchama, M.(2004). *Matumizi ya Taswira na ishara Katika Sauti Ya dhiki*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta, Nairobi. (Hajichapishwa)
- Onyanja, J. W. (2015). *Changamoto za mikondo mipya katika utenzi wa mashairi ya Kiswahili: Mfano Tunu ya Ushairi*. Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta (hajichapishwa)
- Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi, Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: University Press.

Shitemi, N. L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili kabla ya Karne ya Ishirini*. Nairobi: Oxford University Press.

Simpson, P. (2004). *Stylistics. A resource Book for students*. London: Routledge.

Walleck, R., & Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. Hansworth Penguin Books Ltd.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi. Vide-Muwa.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*: Nairobi. Vide-Muwa.